# KUYAANGALIA YASIYOONEKANA

*"Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele". (2Wakorintho 4: 16-18).*

Sikiliza kile Nabii wa Mungu amesema juu ya hilo:

Kuna watu waliokaa hapa usiku huu wa leo ambao walikuwa kwenye viti vya walemavu usiku wa jana au wa juzi. Wameponywa na wanatembea hapa na pale sasa. Inategemea unaangalia nini. Kama unaangalia ugonjwa wako, hutaweza kwenda mbali. Lakini kama unaangalia ahadi ya Mungu, unayo haki ya kila baraka ya wokovu wa Mungu iliyo ahidiwa kwenye Neno lake kuwa yako. Hakika, Mkristo siku zote anaangalia yale yasiyoonekana. [1].

Sasa, njia pekee ambayo waweza kupata kitu chochote kutoka kwa Mungu ni kwa imani. Ninyi nyote mnaelewa hilo? Na sisi kama wakristo, hatuangalii kila tunachoona; tunaangalia kile tunachoamini (2Kor.5:7). Mnaona kile ninachomaanisha? Tunakiamini kabla hakujawa na dalili zozote za kimaumbile [2].

Kila baraka ya Mungu ya wokovu haionekani. Na hapa ndiyo silaha zote za mkristo, upendo, furaha, imani, uvumilivu, utu wema, upole, fadhili, subira. Hayo yote ni nguvu zisizoonekana zikitenda kazi ndani ya moyo wa Muaminio . (Galatia 5:2). Amen. Hiyo ni sawa. Tunaangalia mambo tusiyoyaona. Kama tu watoto wa Ibrahamu, hapo sasa hatuendi kwa kuona, tunaenda kwa imani. Kwa maana Ibrahimu alitembea kwa imani na kuyaita yasiyokuwepo kana kwamba yamekuwepo. Kwa sababu Mungu amesama hivyo (Rumi 4:16 – 22) [1].

Mtu, anapolipata mara moja lile ono la Mungu asiyeonekana na kujua kwamba wakati wote yupo (Matayo 28:20), kuna kitu kinayatuliza mawazo ya huyo mtu; inayatuliza matendo yake, na wakaiti wa shida na mateso, itamfanya yeye bado aangalie juu na juu ya mambo yanayotokea kumzunguka yeye, kwa sababu anaangalia yale yasiyoonekana, na bado ni kwa ahadi [3].

Sasa leo hebu wazia kwamba uwepo wake upo hapa leo. Bwana Yesu yuko kwenye dunia nyingine, au kiwango kingine, hapa hapa leo katika kiwango cha Roho. Roho wake anaungana na roho zetu. Macho yetu hayawezi kumuona Yeye, kwa sababu yako katika hali ya kuonekana bado, labda kuwe na kitu fulani kitokee kitakachotuwezesha kuona maonc ini yupo hapa kama vile vinavyoonekana,



yuko kihalisi tu kama Alivyokuwa siku ile akizungumza na Mariamu kaburini, au alipokutana na Cleopa akiwa njiani kwenda Emmau (Luka 24:13 – 35). Uwepo wake upo hapa unaweza ukasikika na kile, kusikika na ile nguvu iliyowekwa ndani ya mwili wa mwanadamu, inayoitwa kuzaliwa kwa pili, ile nafsi imetiwa nguvu za sumaku kuunganishwa naye.

Na mara moja kwa wakati; unapoacha akili zako zikaze kumuangalia Yeye, kumwamini Yeye, baada ya muda kidogo, uhalisi, unaweza ukasikia kitu fulani kikipita juu ya utu wako. Huo ni ushuhuda wa kufufuka kwake, sio kitu cha kufikiria/"kukisia" siyo "Natumaini hivyo". Lakini kwa kila mtu aliyezaliwa mara ya pili ni kitu "ujuacho kuwa ndivyo hivyo". Ni ……. Unajua hilo. Kiko pale. Na unapokuwa umekutana Naye ……………

Nimewaona watakatifu wakisema, "ooh, unaweza ……. Uwepo wa Bwana uko karibu", Unasema, "kwa nini, kuna kitu fulani…." Kwa nini?, Ni hakika. Yuko hasa pale, sahihi ameinuka….Amefufuka kutoka katika wafu, na Amesimama hasa pamoja na wewe [4].

Sasa, jinsi Ibrahimu, alivyoona siyo yale tu yasiyoonekana. …. Na sababu ya kuamini hilo, ilikuwa ni kwa sababu Mungu amesema hivyo. Na kama tukiwa tumekufa ndani ya Kristo, sisi ni uzao wa Ibrahimu (Galatia 3:29), na kama Roho aliyekuwa ndani ya Kristo anakaa ndani yetu, itafanya jambo lile lile. Itachukua kila ahadi ya kimungu ambayo iko kwenye Biblia Yake na kuifanya iwe ni ya sasa wakati huu, na kupumzika mwenyewe juu ya hilo [3].

Mwanamke huyu mdogo, alikuwa ni myunani, na msirofoinike (Matayo 15:21). Na alikuwa amesikia juu ya sifa za Yesu. Sasa, imani inakujaje? Kwa kusikia, kusikia Neno. Mwanamke huyu alimsikia Yeye. Na unajua, na pengine mwanamke huyu alikuwa na vikwazo vingi vya kumpinga/kumzuia ukizingatia kuwa Yeye ni Myunani. Imani huja kwa kusikia (Warumi 10:17). Tunajua hilo.

Na alikuwa na vitu vingi vya kumpinga Yeye. Lakini imani inatafuta chanzo ambacho hakuna ajuaye chochote juu ya hilo. Imani inatafuta chanzo hicho ambacho hakuna awezaye kukielezea hicho. Ni kitu fulani ambacho unajua wengine hawawezi kukiona, lakini imani inakiona hicho. Imani inakiona hicho ambapo jicho la kawaida halikiri hicho Lakini jicho la ndani linaona jambo hilo (waefeso 1:15 – 18) [6].

Kwa kuwa, unaona, Imani inaona kile Mungu anachotaka kifanyike. Ooh natumaini hili linaingia ndani. Imani haiangalii mambo yaliyopo kwa wakati wa sasa. Imani haioni hili hapa. Imani inaangalia kile Mungu anachotaka, na itatenda sawasawa hasa. Hivyo ndivyo Imani inavyofanya. Inaona kile Mungu anahcotaka, na Mungu anachotaka kifanyike, na imani inatenda kupitia hilo.

Imani ni maono yalengayo mbali. ushi lengo la kuona kwake. Inashikilia kwenye lengo. Amina. Kila aliye aji wa shabaha anajua hilo, kwamba ni

maono ya mbali, kama ni teleskope, au ni binanoklasi/darubini haiangalii hapa; huangalii kwa darubini ili kuona ni saa ngapi unaona? Hutumii hiyo hivyo, lakini unatumia darubini ili kuona mbali, na imani inafanya hivyo. Imani inachukua darubini ya Mungu, zote mbili, sehemu zote mbili, lile Agano jipya na Agano la kale na kuona kila ahadi, ahadi ambayo amiahidi na imani inaiona kule mbali. Na imani inachagua hilo, bila kujali kile ambacho kinasemwa kwa sasa hapa.

Yeye anaangalia kule mwisho. Yeye hashushi lengo lake chini kuangalia upande huu; anaangalia nje kule ng'ambo. Anakiweka kile kilengeo katikati kabisa kwenye Neno. Hivyo ndivyo Imani inavyofanya. Hiyo ndiyo imani ambayo imo ndani ya mtu anayefanya mambo hayo.

Imani inaona kile Mungu anachoona, na mawazo na hisi vinaona vile ulimwengu unavyotaka uone. Angalia, mawazo "Ni nini, ni hisi tu za kibinadamu; Ni mawazo tu ndicho hasa. Vema, "hayo ni mazuri tu." Hivyo ndivyo hasa vilivyo unapotumia hisi hizi zilizo kinyume na Neno, hicho ndicho ambacho dunia inataka wewe uone. Lakini imani haiangalii hilo; imani inaangalia kile Mungu alichosema [7].

Tunaona hilo mara nyingi kuwa watu wanategemea dalili walizonazo, kama wameombewa imani haioni jambo hilo. Imani inaona kile Mungu alichosema. Imani haioni dalili hata kidogo. Imani inakataa kuona dalili. Unasema, "vema, ndugu Branham, kama zipo pale, tusiseme kwamba zipo pale" Hapana hapana, Bwana".

Unasema, "Yeye ni Bwana ambaye ………" ungama/kiri, Yeye ni Kuhani mkuu wa maungamo yetu", Waebrania 3, na yeyote kati yenu ndugu mnajua hilo "kuungama" na "kukiri" ni neno moja hilo. Kwa hiyo Yeye ni Kuhani mkuu wa maungamo yetu (waebrania 3:1-2). Hawezi akafanya chochote mpaka tumekikiri kwanza kwamba amekifanya. (Waebrania 4:14-16) [8].

Kama wewe ni mkristo unasema "kuona ni kuamini" huwezi kuwa mkristo hata kidogo kama unaamini hilo. Kwa maana imani ni hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyo onekana (Waebrania 11:1-2). Huwezi kuwa mkristo na uone kitu chenyewe. Silaha zote za Mungu ni za kimiujiza. Upendo, furaha, amani, imani uvumilivu, wema, unyenyekevu, upole na Roho Mtakatifu vyote hivyo havionekani. Na Mkristo haangalii kile anachoona na macho yake; anaangalia kile anachokiona kwa imani yake. Na imani yake inaweza tu kuwekwa juu ya msingi mmoja tu. Nao ni Neno. Amina [9].

Lakini inategemea ni nini unachoangalia. Unaona nini unapoangalia? Kumbuka, unaweza tu kumuona Yeye kwa kumuangalia kupitia Neno. [10]

Kwa hiyo unaona, lazima uangalie kwenye ahadi za Mungu. Bila kujali kunatokea nini. Angalia kwenye ahadi za Mu siyo unavyojisikia, lakini ni kile Mungu anasema. Sasa, hiyo ni imani ya Ibra 11]



Uzao wa Ibrahimu hauangalii chochote ya vitu hivi vya asili; wanaangalia kile ambacho Mungu amesema (Wagalatia 3:7-9) hiyo ndiyo ahadi. Ni vipi kama Ibrahimu angeangalia yale ya asili, kumuangalia mwanamke wa miaka mia moja, alikuwa na miaka tisini, na yeye Ibrahimu miaka mia moja na ameishi naye tangu ni msichana mdogo na yeye akiwa kijana mdogo, na hakuwa na mbegu? Hakuangalia mambo hayo. Alisema alihesabu mambo hayo kana kwamba hayapo, kwa maana aliangalia tu kile Mungu alichosema. "Nitakubariki wewe, Ibrahimu, nitakupa wewe mzao kupitia Sarah" (Mwanzo 17:15 – 22). Na Yeye aliliamini hilo. Huangalii upinzani; tunaanglaia kile ambacho Mungu amesema. Mungu amesema hilo; hiyo inamaliza yote [12].

Mkristo anaangalia kile ambacho hakioni kimwili. Sasa, angalia. Hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kuwa mkristo. Inakupasa umuamini Mungu, ambaye huwezi kumuona (Yohana 4:24; Waebrania 11:6) Lakini mambo yale ambayo hayaonekani ndiyo mambo yaliyo halisi: mambo yasiyoonekana . [13]

Inategemea unaangalia nini, Biblia, Mkristo, huangalia yale yasiyoonekana, siyo yale unayoyaona hapa. Lakini yale Mungu aliyosema. Hiyo ni ahadi, usijali kile sayansi inasema au chochote kile, ni kile Mungu alichosema.

Unajua, watu wanazungumza juu ya dalili. Nadhani Yona alikuwa na dalili mbaya zaidi ya zote nilizowahi kujua (Yona 2:1-8). Kumbuka, yeye alikuwa katika tumbo la nyangumi. Lakini unajua kile yule nabii alisema? Alikataa kuona tumbo la nyangumi. Alisema "Ni ubatili unaodanganya. Sitaungalia huo" Alisema, lakini mara hii tena nitaliangalia hekalu lako takatifu". Kwa maaana Sulemani alipoliweka wakfu lile hekalu, aliomba, ni mtu, mtu wa dunia hii ambaye baadaye alirudi nyuma. Alipoliweka wakfu lile hekalu la Mungu aliomba, akisema, Kama watu wako wakiwa na matatizo mahali popote na kuangalia kuelekea mahali hapa patakatifu na kuomba, sikia kutoka mbinguni kwako (1Wafalme 9:1-3; 8:28 – 30, 35 – 36). Alikuwa na uhakika kiasi hicho katika maombi ya Sulemani mtu aliye katika jengo la kidunia. [14]

Na kando ya mto Yordani, Mungu alipokuja chini katika umbo la nuru, au hua (njiwa), hakuna aliyona hilo ila Yohana. Watu wote waliosimama kuzunguka hawakuliona hilo. Hakuna aliyeona ila Yohana. Alikuwa mtu pekee aliyekuwa analitazamia, na Mungu alimwambia kwamba angeliona (Yohana 1:29 – 34; Matayo 3:13-17).

Unaona kile unachokitazamia kije. Kama umekuja hapa usiku wa leo kumuangalia Kristo utamuona Yeye.

Kama umekuja kutoa lawama, utakuw kukutosha sana sana mkononi mwako kulaumu/kushutumu. Inategemea unaa nini [15]



Je Yeye si waajabu? Sasa, fikiri, tunamaanisha hilo; kila kitu kimesalimishwa. "Siyo mimi tena katika kufikiria kwangu. Siendi kufikiria kama ambavyo

ningefikiri, Bwana. Nimeenda kufikiri tu kama unavyofikiri wewe. Na umeahidi hilo kwamba nimeponywa (Isaya 53:4-5); Nafikiri hilo. Nimesalimisha mawazo yangu. Sitaenda tenda kufikiri juu ya ugonjwa wangu. Sitaenda kufikiria juu ya ugonjwa niliokuwa nao. Sitaenda kufikiria juu ya chochote ila nifikirie kile ulichosema".

Sasa, mbele yako amesimama mtu kama wewe ulivyo kuwa dakika chache zilizopita; ulikuwa mgonjwa hapa chini. Lakini yupo mtu mzima aliyesimama pale. Yesu Kristo anaita uwe yule mtu mzima aliyevuka hilo. Sasa, kwa imani tu, unapofunga macho yako, tembea kuelekea kwa mtu mwili ule mzima, tena uendelee kutembea tu, uendelee tu kutembea. [16].

Unaona, ni imani yako; kamwe sio kujisikia kwako. Siyo kama iko hivyo kamwe; au kama mkono wangu haukunyooka ………… Hiyo haihusiani kamwe na hilo. Ni imani yangu ndiyo inafanya hilo. Hakika mbele yetu tunaona sura ya mtu mkamilifu aliyeponywa kwa imani. Na sasa basi tunapiga hatua kwa hatua mpaka unaingia ndani ya mtu huyo, na unaendelea tu mbele na hilo. Hakika, hicho ndicho kinachofanya hilo. Imani yako, siyo kujisikia kwako; imani yako inatenda hilo. Ila shukrani na sifa apewe Mungu. [17]

**Nukuu za Kiingereza:**

[1] "Sema na ule mwamba" (60 – 0723),aya 20. [2] Imani pasipo matendo imekufa (50 – 0822), aya 24. [3] Kuyaangalia yasiyo onekana (58 – 1003, Aya 18 – 19 [4] Mtetezi wangu anaishi Aya 47 – 49 [5] Kuyaangalia yasiyo onekana (59 – 0410), Aya 17 [6] Kung'ang'ania (63 – 0113E), aya 42 [7] Kwa nini unalia, Nena (63 – 0714 m), uk. 30 – 31 [8] Matokeo ya uamuzi (55 – 10008) Aya 24 – 25 [9] Tazama (63 – 0428) Aya 46 [10] Tazama aliko Yesu (63 – 1229E)Uk 27 [11] Agano la Mungu na ibrahimu [56 – 0428] Aya 27 [12] Kumiliki malango ya adui 59 – 1108) Aya 42 [13] Mabwana tunataka kumuona Yesu (62 – 0724), Aya 45 [14] Mkuu kuliko Sulemani yupo hapa (61-0412), Aya 72 – 73 [15] Yesu Kristo Yule Yule (63 – 0627) Aya 80 [16] Nenda Kamwamshe Yesu (63 – 1130E) Aya 274 [17] Nimfanyie nini Yesu? (63 – 1124M) aya 34

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 154 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69, D-75328 schomberge, Germany, Simu (+49) 72357613 Fax +(49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*